



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MONDULI

Simu: +255 (027) 2538006 (G/L)
+255 (027) 2538005 (D/L)
Nukushi: +255 (027) 2538136/361
Baruapepe: ded@mondulidc.go.tz
Tovuti: <http://www.mondulidc.go.tz>
Unapojobu tafadhali taja

Halmashauri ya Wilaya,
S.L.P 1,
MONDULI.

Kumb. Na. HW/MON/C5/22 VOLL I/58

19 Juni, 2024

TANGAZO LA KAZI YA MKATABA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli anawatangazia wananchi wote wenye sifa zilizoainishwa kwenye tangazo hili kuomba nafasi za kazi ya mkataba wa miezi mitatu (3) ya ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri.

WAKUSANYA USHURU – NAFASI 24

KAZI NA MAJUKUMU.

1. Kukusanya Mapato ya ndani ya Halmashauri kwa kutumia Mashine za Kielectronic za kukusanya Mapato (POS).
2. Kuhakikisha Fedha inayokusanya inapelekwa Benki katika akaunti za Halmashauri kwa wakati.
3. Kuhakikisha Mapato yote yanayopaswa kukusanya na Halmashauri yanakusanya kwa usahihii.
4. Kutunza kumbukumbu za Hesabu.
5. Kutunza vizuri mashine za kukusanya Mapato (POS).
6. Kutoa na kuwasilisha taarifa za makusanyo ya kila siku kwa Halmashauri.
7. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na msimamizi wake

SIFA ZA WAOMBAJI KATIKA KAZI HII

1. Kuajiriwa wenye Elimu ya kuanzia Kidato cha Nne na kuendelea ambao wana uelewa wa kutumia simu janja (Smart phone), sababu Mapato yote ya Serikali yanakusanya kwa kutumia Mashine za Kielectronic za kukusanya Mapato (POS) ambayo ina application sawa na simu janja. Aidha waombaji wenye sifa zaidi ya zilizotajwa hapo juu maombi yao hayatafikiriwa.

2. Awe ni raia wa Tanzania, Mkazi wa Wilaya ya Monduli
 3. Awe amehitimu kidato cha Nne/sita.
 4. Asiwe Mtumishi wa Umma.
 5. Awe na Umri wa kati ya 18 – 45.
 6. Muadilifu asiye na kasoro yoyote.
-
7. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina mawili ya Wadhamini ambao ni Watumishi wa Umma (Referees), anuani zao sahihi na namba za simu.
 8. Maombi yaambatane pamoja na nakala ya vyeti vyote vya kitaaluma, cheti cha kuzaliwa cha mwombaji na barua za wadhamini.
 9. Awe na kitambulisho cha Taifa /namba ya NIDA.
-
10. Awe tayari kupangiwa kituo chochote cha kukusanya mapato ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Monduli.
 11. Awe muaminifu katika kukusanya mapato ya Serikali na kuhakikisha fedha ya Serikali haipotei.
 12. Awe tayari kutii na kufuata maelekezo atakayopangiwa bila kuvunja misingi ya sheria ndogo za Halmashauri.
 13. Awe na Mdhamsini ambaye ni watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli.

JINSI YA KUTUMA MAOMBI:

Barua zote ziandikwe na kuwasilishwa kuitia anuani ifuatayo;-

MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA,
S.L.P 1,
MONDULI.

TAREHE YA MWISHO YA KUPOKEA MAOMBI NI: 26.06.2024.


Happiness R. Laizer
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
MONDULI.

*MKURUGENZI MTENDAJI
Halmashauri ya Wilaya
ya Monduli*

Halmashauri ya Wilaya, S.L.P 1, Monduli. Simu: +255 (027)-2538006, +255(027) 2538005.
Nukushi +255 (027) 2538136/361. Barua pepe: ded@mondulidc.go.tz. Tovuti: <http://www.mondulidc.go.tz>.